# HABARI ZA KIMATAIFA

## Wachungaji Tanzania kufadhiliwa

**Texas Marekani**

Umoja wa Watanzania Waadventista waishio Marekani (TAUS) unategemea kutumia Dola za Kimarekani 10,000 takribani Tsh 23Milioni kwa ajili ya ufadhili wa masomo ya Uchungaji kwa wanafunzi 10 toka Tanzania kwa Kipindi cha Masomo cha mwaka 2020.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miradi na Ufadhili ya TAUS Mchungaji Caleb Migombo alitanabaisha kuwa kamati hiyo ilipokea maombi ya Watanzania 50 kwa ajili ya ufadhili wa masomo ya uchungaji lakini kamati hiyo imepitisha majina ya waombaji 10 kutokana na sifa na vigezo ambavyo pia vilizingatia bajeti ya mwaka huu ya kutekeleza jambo hilo.

"Watakaonufaika na ufadhili huo ni 6 watakaosomea Uchungaji Katika Chuo Kikuu cha Arusha na wanne watakaosome taaluma hiyo katika Chuo Kikuu cha Bugema cha nchini Uganda". Alisema Mchungaji Migombo.

Mchungaji Migombo aliongeza kuwa, TAUS itaendelea kuwafadhili wanafunzi hao mpaka watakapomaliza masomo iwapo wataendelea kukidhi vigezo vya ufadhili huo kwa mujibu wa taratibu na kanuni za umoja huo ambazo pia huzingatia taarifa muhimu za masomo toka katika vyuo husika.

Taarifa toka Tanzania zinaeleza kuwa kuna uwiano wa Mchungaji mmoja anayehudumia makanisa 10 hasa kwa maeneo ya vijijini, jambo ambalo linawawia vigumu wachungaji kuwahudumia washiriki na pia kufika katika maeneo ambayo kanisa hilo halijapeleka utume wake.

Toka mwaka 2016 hadi 2019 TAUS imesomesha Wachungaji 14 ambapo imekwishatumia kiasi cha Dola za Kimarekani 17,325 ambazo ni sawa na Tsh 39.8Milioni ambazo huchangwa na wanachama wa Umoja huo.

**Shuhuda**

## Maranatha Volunteers kujenga Makanisa na Shule Zambia



**Lusaka, Zambia**

Agano Jipya katika Bibilia limejaa hadithi za mtume Paulo na wamishonari wengine waliosafiri kwa miguu, kwa mashua, na njia zozote za usafirishaji kueneza injili kwa ulimwengu.

Hivi karibuni katika Wilaya ya Shimukuni nchini Zambia, Eddie Himoonde asiye wa mila ya Shumukuni wakati wa kusanyiko la Waadventista wa Sabato 55, alitembea karibu maili 125, bila kupata usafiri.

"Wakati mwingine mimi huchukua labda wiki au wiki mbili tu kwenda kanisani kwa sababu sina gari, sina pikipiki, ninatembea," alisema Himoonde.

"Na wakati mwingine washiriki huja na kunichukua na pikipiki zao kwenda kwa kanisa hilo. Lakini ikiwa hakuna mtu hata aliye na baiskeli katika eneo hilo, basi lazima ninalazimika kulala njiani, nikiamka asubuhi, naendelea kusonga mpaka nifike kwenye kanisa hilo." Aliongeza

Kwa sababu Wilaya ni kubwa na mikusanyiko ni mingi ya kutunza Sabato, Hii hupelekea Himoonde kuona kila kundi mara moja kwa mwaka, anapotembelea, husisitiza mafunzo kwa washiriki kutekeleza kazi bila yeye kuwepo.

Kuna washiriki 11,260 katika wilaya ya Himoonde na wanapenda kuabudu pamoja na kumtukuza Mungu, lakini rasilimali ni duni, na wengi wao hawana jengo la kanisa.

Baadhi yao bado wanaabudu chini ya miti, wengine wao hukata tu nyasi na kufanya makazi karibu, na huanza kuabudu hapo kwa sababu wanampenda Mungu wao.

Washirika wengi wa kanisa wanapenda sana kueneza Injili lakini mara nyingi wanazuiwa kwa ukosefu wa rasilimali na jengo la kuabudia.

"Hii ni changamoto ambayo ninapambana nayo wakati matukio kama haya yanapotokea tunapofanya uinjilisti, na watu wanajitoa kwa Mungu, Lakini wanapokuja kwenye kanisa halisi, wanaona mahali tunakoabudu hapafai, hakuna viti, Wanaabudu chini ya mti au labda kwenye nyasi" Alisema Himoonde.

Mwaka jana, Maranatha Volunteers International, shirika lisilopata faida ambalo linafanya kazi kwa kushirikiana na Kanisa la Waadventista wa Sabato kutoa miundo ya Ibada na elimu ulimwenguni kote, ilianza kujenga makanisa nchini Zambia kwa mara ya pili, baada ya kufanya kazi toka 2009 hadi 2015.

Hivi majuzi, Maranatha walijenga makanisa kadhaa wilayani

"Tayari, watu wanakuja na kuona kinachotokea. Walisikia tu kelele hapa, kazi ambazo zinaendelea. Watu wanauliza, 'Ni nini kinatokea huko? Ni nini kinachotokea hapo? 'Halafu wanaamini kuwa sasa tunamuabudu Mungu wa kweli kwa sababu wametupatia muundo wa kuabudu na Jengo". Na hapo ndipo watu watakuja peke yao. "

Uinjilisti nchini Zambia ni nguvu ya taasisi za elimu ya Waadventista.

Katika jiji la Kabwe kuna shule ya Waadventista moja katika Mkoa huo, na asilimia 65 ya wanafunzi 550 na familia zao sio washiriki wa kanisa.

Kila siku, wanafunzi hufundishwa juu ya Yesu na Mungu anayewapenda, na familia zina hamu ya kuwaandikisha watoto wao kwa sababu ya ufundishaji mzuri wa hali ya juu.

Mnamo mwaka wa 2018, Maranatha Volunteers International ilikubali kujenga kambi mpya ya shule ya Msingi Kabwe, ambayo itatoa nafasi zaidi kwa wanafunzi wa sasa na kutoa watoto zaidi fursa ya elimu ya Adventist.

Ujenzi ulianza mnamo 2019, na wafanyakazi wa kujitolea 132 kusaidia kujenga majengo nane, pamoja na ofisi ya utawala.

## China kudhibiti Corona

**Beijing, China**

Mkurugenzi mkuu wa shirika la afya duniani WHO Tedros Adhanom Ghebreyesus, amesema kuwa ana imani kuhusu uwezo wa China wa kudhibiti kusambaa kwa virusi vya Corona.

Hii ni kwa mujibu wa shirika la habari la serikali ya China, Xinhua. Katika mkutano na maafisa wa serikali ya China mjini Beijing, Tedros amesema ameidhinisha hatua za serikali ya China za kukabiliana na mripuko huo kufikia sasa.

Tedros pia amesema hashauri kuondolewa kwa raia wa kigeni nchini humo ambao kwasasa wako



China na kuwahimiza watu kuwa watulivu.

Idadi ya waliofariki kutokana na virusi hivyo imeongezeka kufikia watu 106 nchini China na visa vinavyoongezeka vinaripotiwa katika mataifa mengine.

## Netanyahu aondoa kinga ya mashtaka

**Jerusalem, Israel**

Waziri mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu ameondoa ombi lake la kinga dhidi ya mashtaka saa chache kabla ya kuanza kwa vikao vya bunge.

Bunge la Israel lilitarajiwa kuandaa kikao cha kuzungumzia kubuniwa kwa kamati ya kujadilia ombi hilo la waziri mkuu la kinga ya mashtaka.

Netanyahu alishtakiwa kwa makosa ya ulaghai, kuvunja uaminifu na hongo mnamo mwezi Novemba katika visa vitatu tofauti. Hata hivyo amekanusha mashtaka hayo.

## Wafungwa, wahudhuria bunge Catalonia

**Barcelona, Spain**

Watu sita waliokuwa wanachama wa serikali ya Kanda ya Catalonia wamesafirishwa kutoka gerezani kuhudhuria kikao cha bunge mjini Barcelona.

Aliyekuwa makamu wa Rais wa jimbo hilo Oriol Junqueras na wenzake watano waliokuwa mawaziri ambao wote wanatumikia vifungo gerezani kutokana jaribio la mkoa huo kujitenga na Uhispania, walipokelewa kwa shangwe na nderemo za "uhuru" na kundi dogo la watu ndani ya jengo.

# HABARI ZA KIMATAIFA

## WHO: Visa vya maambukizi vyapungua Italia na Uhispania

**New York, Marekani**

Shirika la afya duniani limesema kuwa visa vya maambukizi ya virusi vya Corona vinapungua nchini Italia na Uhispania tofauti na Uingereza, Uturuki na Marekani ambapo visa vya maambukizi vinazidi kuongezeka.

Shirika hilo lilisema kuwa, asilimia 90 ya visa vipya vya maambukizi ya virusi vya Corona kwa sasa hivi vinatokea Ulaya na Marekani na wala sio China, ambayo ilikuwa kitovu cha maambukizi ya virusi hivyo.




Msemaji wa WHO Dkt. Margaret Harris alisema hayo akiwa Geneva na kuongeza kuwa visa vipya vya maambukizi nchini China vinaletwa na wageni.

Vilevile aliongeza ulimwengu usitarajie chanjo dhidi ya virusi vya Corona katika muda wa mwaka mmoja au hata zaidi.

Naye katibu mkuu wa Jumuiya ya kujihami NATO Jens Stoltenberg alizitaka nchi wanachama wa muungano huo kuchukua janga la virusi vya Corona kama funzo ili kuongeza vifaa vya matibabu badala ya kutegemea misaada ya nje.

Stoltenberg amesema hayo siku moja tu kabla ya mkutano wa mawaziri wa ulinzi wa nchi wanachama wa Nato utakaofanyika kwa njia ya video.

Aliongeza kuwa mkutano huo utajikita zaidi katika suala la kuongeza ushirikiano kati ya nchi wanachama hasa kwa usafirishaji wa vifaa vya matibabu kwa sehemu zinazohitajika zaidi.

Na nchini Iran, idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa wa COVID-19 imepungua kwa mara ya kwanza mwezi huu.

"Tumeweka vikwazo vya usafiri kati ya wilaya moja hadi nyingine kote nchini. Mungu akipenda, tunapanga kuondoa vikwazo hivyo ifikapo Aprili 20" alisema Rais wa Iran Hassan Rouhani.

Msemaji wa wizara ya afya nchini humo Kianoush Jahanpour alisema kuwa watu 98 wamekufa kutokana na ugonjwa wa COVID 19 katika muda wa saa 24 zilizopita na kufikisha idadi jumla ya watu waliofariki kwa ugonjwa huo kuwa 4,683.

Jahanpour aliongeza kuwa watu wengine 1,574 wamepatikana na virusi vya Corona na kufikisha idadi jumla ya watu walioambukizwa virusi hivyo kuwa 74,877.

Na huko nchini Uhispania na Austria, mamlaka zimeruhusu japo kwa kadri watu kuanza kurudi kazini kinyume na Ufaransa na India ambazo zimerefusha muda wa usitishaji wa shughuli ili kukabiliana na kuenea kwa virusi vya Corona.

Nchini Uhispania, vikwazo vimesaidia kupunguza kasi ya maambukizi na idadi ya vifo ambavyo vilikuwa vimefikia kilele chake mapema mwezi huu wa Aprili. Nchi hiyo imerekodi idadi ndogo ya maambukizi mapya tangu Machi 18.

Hata hivyo, baadhi ya wafanyakazi wameonyesha wasiwasi wao juu ya kulegeza vikwazo hivyo wakisema huenda kukashuhudiwa mlipuko mwengine.

## Watanzania Waadventista waishio Marekani watakiwa kuondoa hofu



**Watanzania waishio nchini Marekani wakiwa katika picha ya Pamoja.** PICHA NA MAKTABA

**Na Emanuel Maduhu, Huston Texas**

Makamu Mwenyekiti wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Duniani Mchungaji Geofrey Mbwana amewaasa Watanzania Waadventista waishio Marekani wenye umoja wa TAUS kuondoa hofu iliyotanda kutokana na janga la Virusi vya Corona lililozikumba nchi nyingi Duniani huku Marekani ikionesha idadi kubwa ya visa vya ugonjwa huo.

Umoja wa Watanzania Waadventista waishio Marekani TAUS ulioanzishwa mwaka 1999 una idadi ya wanachama hai 350 kutoka majimbo 50 nchini humo ambako kuna idadi ya watu zaidi ya milioni 329 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2019 za kituo cha sensa cha Marekani, huku kukiwa na taarifa za wanachama wawili wa umoja huo waliougundulika na virusi vya Corona ambao hali zao kwa sasa zinaendelea vizuri baada ya kupata matibabu.

Makamu Mwenyekiti aliyasema hayo katika hotuba yake ya faraja aliyoitoa kwa njia ya mtandao wa intaneti kupitia Program tumishi ya Zoom ambayo iliwaunganisha wana TAUS wapatao 150 wakiwa na familia zao.

"Janga la Corona ni jaribu lingine kubwa ambalo linahitaji ujasiri wa kukabiliana nalo kwa kumtegemea MUNGU huku tukizingatia kanuni na taratibu za kujikinga na kujilinda na ugonjwa wa Covid-19 zinazotolewa na mamlaka za Afya nchini Marekani", alisema Mchungaji Mbwana.

Hii ilikuwa ni mara ya pili kwa Uongozi wa TAUS kuwakutanisha wanachama wake walioko katika majimbo mbalimbali kwa Ibada ya Siku ya Sabato ambayo ilihusisha maombi, hotuba, nyimbo na shuhuda kwa njia ya teknolojia ya intanet kupitia zoom, jambo ambalo awali kabla ya Karantini lilikuwa likifanyika kwa viongozi wa TAUS pekee kwenye kikao chao ambacho hufanyika mara moja kwa mwezi.

Naye Chaplesia wa chama hicho Mchungaji Caleb Migombo alisema utaratibu wa Ibada kwa njia ya Mtandao utasaidia sana kuleta umoja, kutiana moyo na kuondoa msongo unaotokana na upweke katika wakati huu ambapo kuna hofu na upweke miongoni wa wanachama kutokana na karantini iliyowekwa nchini Marekani.

Serikali ya Marekani imewaweka karantini wakazi wake kwa mwezi mmoja sasa ikiwa ni jitihada ya nchi hiyo katika kukabiliana na janga la Virusi vya Corona lililoikumba dunia kwa sasa ambapo mikusanyiko yote ya watu 10 na kuendelea imezuiwa nchini humo ikiwemo kuhudhuria katika nyumba za Ibada hali ambayo imesababisha madhehebu kuendesha ibada kwa njia ya mtandao wa intaneti.

# HABARI ZA KIMATAIFA

## COVID-19: Rais Kenyatta aitisha kikao



**Nairobi, Kenya**

Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya ameitisha kikao maalum cha kilele na magavana kitakachofanyika siku ya Ijumaa kufuatia ongezeko la visa vya ugonjwa wa COVID-19

Kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, Rais Kenyatta alisema kuwa kikao hicho kitatathmini utayari wa majimbo kukabiliana na virusi hivyo. Taarifa hiyo imesema kuwa, kweye kikao hicho watazangalia mbinu za matibabu ya ugonjwa huo na jinsi ugonjwa huo utakavyokuwa umesambaa katika miezi ya Agosti na Septemba.

Jimbo la Tana River limekuwa jimbo la karibuni zaidi kuripoti visa vya virusi hivyo na kuongeza idadi ya majimbo yenye visa hivyo kuwa 44 kati ya 47.

Serikali imeonesha wasiwasi wa ongezeko la virusi

Waziri wa Afya Mutahi Kagwe alieleza wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa visa hivyo kila siku. Kenya imerikodi jumla ya visa 13, 770 mpaka sasa, baada ya visa vingine 400 kuripotiwa juzi.

Na katika hatua nyingi soko la maua nchini humo limeanza kupata nuru kwa kiwango cha asilimia 85 katika kipindi hiki ambacho soko la Ulaya linafunguliwa baada ya vizuizi vya kukabiliana na janga la corona.

Taarifa ya sekta hiyo muhimu ya kibiashara inaonesha Kenya itaingia katika muendelezo kamili wa ufanyaji biashara kwa mwaka ujao. Wakulima wa Kenya walilazimka kuitelekeza shehena ya maua yao baada ya mataifa mengi ya Ulaya kuifunga mipaka yao mwezi Machi na wakazi kuwekewa masharti katika shughuli za mazishi na harusi.

## Maandamano ya Portland: Trump atishia kupeleka wanajeshi katika miji mingi zaidi

**New York, Marekani**

Rais Donald Trump ametishia kutuma maafisa wa jeshi katika miji mingi zaidi Marekani kudhibiti maandamano yanayoendelea.

Bwana Trump aliikosoa miji kadhaa inayoongozwa na chama cha "liberal Democrats'', ikiwemo Chicago na New York, akisema kuwa viongozi wanaogopa kuchukua hatua.

Alisema kuwa maafisa waliotumwa Oregon walifanya kazi nzuri ya kurejesha amani huku kukiwa na siku kadhaa za maandamano eneo la Portland.

Hata hivyo, maafisa wa eneo walisema kuwa maafisa wa serikali wanafanya hali kuwa mbaya zaidi.

Viongozi wa majimbo wametaka Bwana Trump kuondoa maafisa alioagiza kupelekwa huko Portland na kumshutumu kwa kufanya hali kuwa mbaya zaidi kama njia ya kutafuta ushawishi wa kisiasa mwaka wa uchaguzi.

Akizungumza katika Ikulu ya Marekani, Trump alirejelea wito wa utekelezaji sheria na utaratibu.

"Tunatuma vikosi," aliwaambia wanahabari. "Hatuwezi kuacha hili liendelee kutokea katika miji."

Alitaja miji ya New York, Chicago, Philadelphia, Detroit, Baltimore na Oakland akiwa anazungumzia matatizo yatokanayo na ghasia.



"Hatuwezi kuacha hili litokee katika nchi yetu, yote ni maeneo yanayoongozwa na chama cha liberal Democrats."

Trump pia alipongeza juhudi za maafisa hao waliosababisha utata kwa kutekeleza sheria huko Portland. Mji huo umekuwa ukishuhudia maandamano dhidi ya unyama unaotekelezwa na polisi mjini humo tangu kutokea kwa mauaji ya George Floyd, mwanaume mweusi huko Minnesota Mei.

Hata hivyo Trump alituma maasifa wa serikali katika hilo la magharibi mwa pwani ya Marekani wiki mbili zilizopita kutuliza maandamano hayo.

Baadhi ya maafisa wametumia magari ya kawaida na kusababisha ukosoaji mkubwa kutoka kwa Democrats na wanaharakati.

Wiki iliyopita, wasiwasi kati ya waandamanaji na maafisa hao wa polisi umeongezeka na viongozi wa eneo wametoa wito kuwa maafisa hao wa serikali kuu waondoke mjini humo.

Trump alisema kuwa gavana wa Oregon, meya wa Portland na viongozi wengine wa majimbo wanaogopa raia hao aliowataja kama wanaopinga serikali.

"Wanaogopa watu hawa," alisema. "Hiyo ndiyo sababu hawataki sisi tuwasaidie."

Meya wa Chicago Lori Lightfoot awali alisema ana wasiwasi kwa hatua ya Trump ya kupeleka maafisa wa serikali mjini humo. Aliongeza kuwa alizungumza na meya wa Portland ili kupata uelewa zaidi wa kile kinachoendelea.

"Hatutaki maafisa wa serikali bila taarifa zozote wanaochukua watu barabarani na kuwakamata, nafikiri hilo ni kinyume cha sheria," Bi. Lightfoot alisema.

Akizungumza na CNN, meya wa Portland Ted Wheeler alisema kuwa 'kuna wanajeshi kadhaa ikiwa sio mamia' mjini humo, na kuongeza kuwa "Uwepo wao unafanya kuwe na maandamano na uharibifu zaidi wa mali.

Aidha mwanasheria mkuu wa Oregon amewasilisha keshi dhidi ya serikali kuu kwa kuwakamata waandamanaji kinyume cha sheria na kukiuka haki ya kikatiba.

## TAUS yatoa Milioni 12 kufadhili wainjilisti walei

**Na Emmanuel Maduhu, Huston Texas**

Umoja wa Waadventista Watanzania waishio Marekani (TAUS) unatarajia kutumia kiasi cha Tsh 12 Milioni kwa ajili ya gharama za kujikimu kwa wainjilisti walei 10 nchini Tanzania kwa muda wa miezi sita.

Wainjilist hao walei wanatarajiwa kutoa huduma za malezi ya kiroho kwa waumini wapya waliobatizwa katika Mkutano wa Mungu Kwanza Chato 2020 uliomalizika mwanzoni mwa mwezi Machi mwaka huu.

Kikao cha Kamati ya Utendaji ya TAUS kilichofanyika hivi karibuni kilipitisha fedha hizo zitakazoelekezwa kwa mradi huo ambao utaratibiwa na Jimbo Kuu la Kaskazini mwa Tanzania NTUC, na wainjilist hao 10 watahudumia washiriki hao wapya katika mitaa ya Chato Central, Ikorogo-Serengeti, Makao, Mwamapalala, Loliondo, Moronjoda, Lwamgasa, Butundwe, Simanjiro na Hai-Siha.

Mkutano wa Chato 2020 Mungu Kwanza uliendeshwa kwa majuma matatu na Kanisa la Waadventista nchini Tanzania huko Chato mkoani Geita na ulidhaminiwa na TAUS kwa kushirikiana na Chama cha Wajasiriamali na Wanataaluma Waadventista Tanzania ATAPE.

Mkutano huo ulirushwa na vyombo vya habari vya Kanisa Tanzania, Mhutubu akiwa ni Mchungaji na Dkt. Carlton Byrd toka Marekani na watu 15,556 walibatizwa.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1999 nchini Marekani, TAUS ina wanachama hai wapatao 350 toka majimbo mbalimbali nchini humo na imekuwa ikijihusisha na miradi mbalimbali ya Uinjilisti na Kijamii nchini Tanzania ikiwemo, kusomesha wachungaji, Huduma za Afya, ujenzi wa makanisa na kusaidia vyombo vya Habari.

## EU yafikia makubaliano ya bajeti yao

**Brussels, Belgium**

Viongozi wa Umoja wa Ulaya wamemaliza mkutano wao wa kilele uliochukua siku nne za majadiliano makali na kushangilia kile wanachojiaminisha kuwa ni mpango wa kihistoria wa uokozi kwa ajili ya uchumi wa mataifa yao ulioharibiwa na janga la virusi vya corona.

Makubaliano ya euro bilioni 750 yalifikiwa baada ya majadiliano makali ambayo yalishuhudia wajumbe wa Ufaransa wakitoka nje na huku kura ya turufu ikipigwa na Hungary, upinzani mkali kutoka Uholanzi na Austria kwa mpango huo.

Mkuu wa baraza la Ulaya Charles Michel ambaye aliongoza majadiliano hayo yaliyochukua zaidi ya masaa 90, alisema yalikuwa majadiliano magumu katika nyakati za matatizo makubwa kwa Ulaya.

# HABARI ZA KIMATAIFA

## UN: Beiruti ina mahitaji lukuki ya kibinadamu



**Geneva, Uswisi**

Mashirika ya Umoja wa Mataifa yameonya kwamba mahitaji ya haraka ya kibinadamu nchini Lebanon ni makubwa sana kufuatia mlipuko mkubwa uliosambaratisha bandari ya mji wa Beiruti.

Duru za hivi karibuni zimesema takribani watu 150 wamepoteza maisha na maelfu kujeruhiwa lakini idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka, wakati huu ambapo waokozi wanaendelea kusaka manusura kwenye vifusi.

Msemaji wa shirika la afya la Umoja wa Mataifa WHO Christian Lindmeier amesema kwamba watu wengi bado hawajulikani waliko na kwamba hospitali zimezidiwa uwezo.

Akizungumza na waandishi wa Habari kwa njia ya video mjini Geneva Uswisi ameongeza kuwa vituo vitatu vya afya havifanyi kazi na viwili vingine zimeharibika kiasi na kwamba janga hilo limesambaratisha kabisa vitanda 500 vya hospitali.

"Kipaumbele cha sasa ni huduma ya wagonjwa mahututi na kusaka na kuokoa manusura bila shaka , hilo ni la muhimu sana, bado kuna watu wamenasa katika kifusi na bado kuna watu wako hai chini ya kifusi hicho kulingana na tunayoshuhudia katika vyombo vya Habari na hicho ndio kipaumbele chetu cha kwanza kwa sasa, na bila shaka kuingiza vifaa na misaada, chakula, malazi, pia madawa, vifaa tiba kwa ajili ya wagonjwa mahtuti na pia kwa ajili ya magonjwa yote ambayo hayawezi kutibiwa hospitali kwa sasa", alisema Landmeier.

Wakati kukiwa na hofu kuhusu vumbi hatari lililosababishwa na mlipuko huo wa tani 2,750 za gesi ya ammonium nitrate, msemaji huyo wa WHO amewaambia waandishi wa Habari kwamba wizara ya afya ya Lebanon iliarifu kupungua kwa kiwango cha sumu saa mbili baada ya mlipuko huo.

Katika suala hilohilo shirika la Umoja wa Mataifa la mpango wa chakula duniani WFP limetangaza kwamba litaingiza unga wa ngano na nafaka ili kusaidia kuinua hali ya uhakika wa chakula nchini Lebanon wakati nchi hiyo ikijikita katika ujenzi mpya wa bandari ya Beiruti ambako maghara makubwa ya nafaka yamesambaratishwa.

Utafiti wa hivi karibuni wa umebaini kwamba chakula kimekuwa chanzo kikuu cha hofu nchini Lebanon tangu kutangazwa kwa hatua za kufunga kila kitu kutokana na COVID-19, ambapo mtu 1 kati ya 2 anahofia kutokuwa na chakula cha kutosha.

Ili kusaidia walio hatarini zaidi shirika hilo linatenga makasha 5,000 ya chakula kwa ajili ya familia zilizoathirika na mlipuko. Kila kasha linatosheleza kulisha familia ya watu watano kwa mwezi mzima likiwa na vyakula vya msingi kama mchele, kunde, makopo ya samaki jotari, chumvi na nyanya za makopo.

## Idara ya Elimu nyenzo kongwe ya uinjilist wa kiadventista

**Na Maduhu Emmanuel Texas, Marekani**

Waumini wa Kanisa la Waadventista wa Sabato wametakiwa kuwekeza katika idara ya elimu kwa kuwa ni nyenzo kongwe na muhimu katika kupeleka utume wa kanisa hilo duniani.

Mkurugenzi wa Idara ya watafuta njia ya Kanisa hilo katika Konferensi ya Kaskazini mwa Uingereza (NEC) Mchungaji Ikwisa Mwasumbi, alitoa agizo hilo wakati akitoa hotuba yake fupi toka nchini Uingereza kwa Watanzania Waadventista waishio Marekani wakati wa kuhitimisha juma la maombi la TAUS 2020 lililoendeshwa kwa njia ya mtandao wa zoom.

"Jambo moja ambalo naweza kusisitiza kwa wazazi ni kwamba tuamke tuangalie nini cha kufanya kwa watoto wetu kwa kuwa ni mahali ambapo tunaweza kuwekeza kwa kuwapa mafundisho yenye mtazamo wa Kanisa letu", alisema Mchungaji Mwasumbi.

Mchungaji Mwasumbi alieleza kuwa, kuwepo kwa shule za kiadventista kumechangia ukuaji wa Kanisa la Waadventista wa Sabato duniani kwani mwaka 1880 kanisa hilo lilikuwa na shule mbili tu za vijana na wainjilisti watano,mwaka 1990 kukawa na shule 245 na kuwa na idadi ya wainjilisti 481,idadi hiyo iliongezeka mwaka 1930 ambapo shule zilikuwa 2,178 na kukawa na wainjilisti 8,479.

Takwimu za Kanisa la Waadventista wa Sabato zinaonesha kuwa kumekuwa na matokeo chanya ya ongezeko la idadi wanafunzi vijana wanaobatizwa katika shule za Kanisa hilo kila mwaka toka mwaka 2006 ambapo idadi ilikuwa 30,778 wakati idadi hiyo iliongezeka na kufikia waumini 43,475 waliobatizwa katika shule hizo kwa mwaka 2015.

Hadi kufikia Disemba 31 mwaka 2017 Kanisa hilo lilikuwa na shule 8,540 kati ya hizo shule za msingi zilikuwa 5,943 zikiwa na wanafunzi 1,183,337 ambapo shule za sekondari zilikuwa 2,429 ambapo kulikuwa na idadi ya wanafunzi 595,848 katika shule hizo.

Katika hatua nyingine Mchungaji Mwasumbi aliwapa changamoto wazazi na walezi walioko ughaibuni kuwahusisha watoto wao katika miradi mbalimbali ya kiunjilisti wanayoifanya nyumbani kwa kufanya hivyo ni njia moja ya kuwafanya watoto hao watambue wanajenga kanisa lao na kuwafanya wadumu katika imani.

## Uingereza na Ufaransa kushirikiana ili kukomesha uhamiaji haramu

**London, Uingereza**

Uingereza imedhamiria kushirikiana na Ufaransa ili kuzuia boti ndogo zinazobeba wahamiaji kuvuka eneo la maji baina ya nchi hizo na kuingia nchini Uingereza.

Hayo yalisemwa na waziri mdogo wa Afya wa Uingereza Edward Argar wakati akizungumza na kituo cha redio cha LBC juzi Jumanne 11 Agosti 2020.

Argar alikiambia kituo hicho cha redio kuwa, Uingereza itafanya kazi kwa ushirikiano na Ufaransa ili kukomesha safari hatari za wahamiaji ambazo pia ni kinyume cha sheria.

Wafanyabiashara haramu wa wanaosafirisha wahamiaji wamekuwa wakitumia boti zinazowasafirisha wahamiaji wanaotaka kufika Ulaya kupitia njia ya bahari ili kutafuta maisha bora.

## Tunisia: Waziri mkuu kuteua watu wasio wanasiasa kuwa mawaziri



Waziri Mkuu mteule wa Tunisia Hichem Mechichi.

**Tunis, Tunisia**

Waziri mkuu mteule nchini Tunisia amesema kwamba ataunda baraza la mawaziri lenye watu ambao sio wanasiasa kufuatia mzozo usiomalizika kati ya vyama vya kisiasa kuhusu uundwaji wa serikali mpya.

Hatua ya Hicehm Mechichi, huenda ikamuweka katika hali ya mvutano na chama cha Ennahda chenye wabunge wengi na ambacho tayari kimesema kwamba kitapinga kabisa hatua yoyote ya kuteua serikalini watu ambao sio wanasiasa.

Hata hivyo pendekezo la kuunda serikali ya wataalam wasioegemea kundi lolote la kisiasa huenda likapata uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa muungano wa wafanyakazi wenye nguvu sana nchini Tunisia -UGTT, Pamoja na vyama vingine vya kisiasa, vikiwemo Tahya Tounes na Doustoury el Hor.

Mechichi alisema kwamba lengo la serikali litakuwa kutatua hali ngumu ya maisha wanaopitia watu wa kawaida na kujenga uchumi ambao umeharibika.

Amekashifu wanasiasa kwa kuzozana wakati raia wa kawaida hata hawana maji safi ya kunywa.

Maandamano yametokea katikati mwa Tunisia mwaka huu kulalamikia ukosefu wa ajira na huduma mbovu serikalini hasa za afya, ukosefu wa maji na umeme.